# HADHI NA DHIMA YA VIUNGANISHI KATIKA MIUNDO YA KISWAHILI

*Y .M. Kihore*
*Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam*

## 1.0 Utangulizi

Nia yetu katika makala hii ni kuchunguza hadhi na dhima ya viunganishi vinapokuwa katika miundo mbalimbali ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kutokana na tatizo kwamba kanuni iliyokitwa katika misingi ya kiunzi cha nadharia ya Sarufi Geuza-maumbo Zalishi ambayo imekuwa ikitumiwa katika uchanganuzi wa miundo mbalimbali yenye viunganishi haionekani kuwa toshelevu. Kanuni hii ni ya aina inayoonekana katika (1) hapa chini:

1. $\alpha \rightarrow \alpha_1 \ldots \{na\}\ \alpha_n$

ambako $\alpha$ ni kategoria yoyote ile.

Katika kiunzi hiki cha nadharia kilichotawalia, kanuni hii ilikuwa ikitumiwa pamoja na kanuni nyingine mbili ambazo ni (a) kanuni ya Utendwa inayopanga miundo katika sentensi tu na si katika virai vitenzi, na (b) kanuni geuzi ya Kipunguza Uunganisho (*Coordination Reduction*) iliyobuniwa kuchanganua miundo yote yenye viunganishi ikiwa na uwezo wa kufuta vipashio vinavyofanana na kuvipanga pamoja vile vilivyobaki. Hivyo, kutokana na kanuni katika (1) kutumiwa sambamba na kanuni ya Utendwa ilidhihirika kuwa haiwezi (taz. Schachter 1976:236-237) kuzalisha muundo wa virai vitenzi vilivyounganishwa katika sentensi ya lugha ya Kiingereza katika (2):

2. *The Dodgers beat the Red Sox and were beaten by the Giants*

Sentensi katika (2) ina pengo kutokana na kutorudiwa kwa Kikundi Nomino (KN) *The Dodgers* baada ya kiunganishi *and* na kubakiza kirai kitenzi *were beaten by the Giants* upande wa kulia. Hii ina maana kanuni hii haikuweza kuchanganua miundo yenye mapengo yenye viunganishi.


Aidha, ili kuzalisha sentensi kama hiyo katika (2), kulihitajika kanuni ya Kipunguza Uunganisho ambayo kazi zake zimeelezwa hapo juu. Hata hivyo, kanuni hii ilitoa madai mazito kuhusu sentensi zilizounganishwa zenye mapengo (taz. Gazdar 1980; Keenan na Faltz 1978), lakini ikashindwa hata kutabiri (Gazdar 1981:157) kuwa sentensi ya Kiingereza katika (2) inahusiana katika maana na sentensi nyingine hii ya Kiingereza katika (3):

3. *The Dodgers beat the Red Sox and the Dodgers were beaten by the Giants*

Matatizo haya yalidhihirisha kwamba kanuni hii kuu haikuwa toshelevu katika uchanganuzi wa miundo iliyounganishwa kwa viunganishi.


Katika lugha ya Kiswahili, kanuni katika (1) imekuwa ikitumiwa kuchanganua miundo hasa ile katika (4) na (5) hapa chini bila kutilia maanani kwamba kuna mambo mengi changamani yanayohusika hata katika miundo hii ambayo inaonekana kuwa ya msingi na ya kawaida kuliko ile inayofanana na hiyo ya Kiingereza katika (2) na (3). Hebu tuitazame miundo hiyo na jinsi ilivyochanganuliwa kwa kanuni hiyo:

4. Muundo wa Kirai Nomino (KN) wenye kiunganishi: KN → N U N
   (a) Baba na mama
   (b)




Muundo katika (4) ni ule wa Kirai Nomino. Uchanganuzi katika (4b) unaonyesha kwamba vipashio *baba, na* na *mama* vinamilikiwa kwa namna iliyo sawa, yaani vyote vinamilikiwa moja kwa moja na KN. Swali la kujiuliza hapa ni, je, hii ina maana gani katika mahusiano ndani ya kirai ambayo, kwa kawaida, hutegemezwa katika neno kuu? Swali jingine ni je, katika hali hiyo, kiunganishi kina hadhi gani – ni neno kuu, sehemu yake au ni mojawapo tu ya vijalizo?

5. Muundo wa Sentensi (S) Ambatani wenye kiunganishi: S → $S_1$ U $S_2$
   (a) Mama anafagia na watoto wake wanacheza nje
   (b)




Katika (5), uchanganuzi katika (5b) nao unaonyesha kuwa kipashio Sentensi (S) kinamiliki $S_1$, *na* na $S_2$ kwa namna iliyo sawa, yaani moja kwa moja. Hapa pia kiunganishi kinamilikiwa kwa namna sawa na vipashio vilivyo vikubwa kwake kimiundo. Katika

hali hii napo swali ni, je, kiunganishi kina hadhi gani katika mahusiano haya ndani ya (S) – ni kishazi kama vipashio vyenzie katika muundo huo au ni neno? Na kama ni neno au kipashio kingine tofauti, kwa nini kimilikiwe kwa namna sawa na vishazi?

Kwa kutumia kanuni katika (1) kuchanganua miundo katika (4) na (5), kwanza tunapata matokeo yaliyo sawasawa kuhusiana na hadhi na dhima ya kiunganishi na, kwani katika miundo yote miwili kipashio hicho kina dhima ileile ya uunganishi na vilevile hadhi ileile ya kuwa aina ya neno japokuwa kiko miongoni mwa vipashio vya hadhi tofauti kimiundo. Lakini cha pili na ambacho tunafikiri ni muhimu zaidi kwa malengo ya makala hii ni mahusiano ndani ya miundo hiyo yanayotabiriwa na kanuni hiyo na hasa kwa kuzingatia hadhi ya kiunganishi. Yote haya yana maana kwamba uchanganuzi wa kipashio kiunganishi kwa kutumia kanuni katika (1) una matatizo kuhusiana na muundo wa msingi kabisa kama ule wa KN katika (4), muundo usio na pengo kama wa S katika (5), na miundo yenye mapengo kama tulivyoona kuhusiana na miundo ya Kiingereza katika (1) na (2). Tatizo hili Gazdar (1981:158) ameliita tatizo la kuipa miundo yenye viunganishi "umbo la nje ambalo si sahihi".

Makala hii itachunguza tatizo lililojitokeza kuhusiana na uchanganuzi wa miundo katika (2) -(5) uliokitwa katika kanuni katika (1) na kuona mapendekezo mengine kuhusu jinsi ya kuchanganua miundo mbalimbali yenye viunganishi. Tutaanza kwa kutoa usuli wa kinadharia na kisha kutazama miundo mbalimbali yenye viunganishi katika Kiswahili na jinsi inavyoweza kuchanganuliwa kwa kanuni nyingine zinazopendekezwa.

## 2.0 Usuli wa Kinadharia

Kama tulivyodokeza katika sehemu iliyotangulia, uchanganuzi wa miundo yenye viunganishi kwa kutumia kanuni katika (1) juu ndiyo imetawala katika changanuzi mbalimbali za miundo yenye kipashio hiki katika Kiswahili. Hii, kama tulivyoona inaibua tatizo lenye kuhusu hasa hadhi ya kipashio kiunganishi katika miundo hiyo kwa kutoonekana wazi sababu za kimiundo za kufanya kipashio hicho nacho kimilikiwe sawasawa na vipashio vingine vinavyohusika katika muundo. Lakini cha muhimu zaidi hapa ni kuendelea kutumika katika Kiswahili kwa uchanganuzi unaotumia kanuni katika (1) wakati Ross (1967:90-91) aliwahi kuonyesha kwamba "kuna sababu za kifonolojia na za kisintaksia za kufanya iaminike kwamba neno linalounganisha [vipashio vya miundo] ni sehemu ya kipashio katika kifundo kinachofuata na si tu 'dada' kwa vifundo vyote vinavyohusika" (tafsiri yangu). Katika maelezo haya ya Ross, "udada" unahusu mahusiano kama yale yanayoonekana katika (4) na (5) ambamo vipashio vyote vinavyohusika katika muundo humilikiwa moja kwa moja na kipashio kikubwa, yaani kipashio KN (katika (4)) na kipashio S (katika (5)); ikiashiria kuwa vina hadhi sawa kimiundo. Hii ina maana kwamba kwa minajili ya mtazamo wa Ross, katika (4) mbinu mbalimbali za kinadharia zenye kuweza kukabili uchanganuzi wa miundo kama hii ambayo ni ya aina nyingi katika lugha kama itakavyoonyeshwa katika sehemu inayofuata.

kiunganishi **na** kilipaswa kuwa sehemu ya kipashio "mama" kilicho upande wa kulia na katika (5) kiunganishi kilipaswa kuwa sehemu ya kifundo ($S_2$) cha upande wa kulia chenye maneno "watoto wake wanacheza nje". Au kwa kifupi ni kwamba kiunganishi katika miundo kama (4) na (5) hapo juu hakistahili kumilikiwa peke yake moja kwa moja na vipashio vikuu KN na S. Lakini mtazamo huu ulihitaji ubunifu wa mtazamo wa Ross wa kukabili miundo yenye viunganishi ulitiliwa maanani na kiunzi cha nadharia cha Sarufi Miundo Virai Changamani. Kiunzi hiki, kwa kuzingatia dhana mbalimbali zinazofungamana na miundo yenye viunganishi **na** kwa kuchukulia kwamba hakuna ugeuzi, kilibuni kanuni mbili: moja inayoingiza kiunganishi kama sifa kwenye kifundo kinachokifuata na nyingine inayopanua muundo uliojumuisha kipashio hicho, zinazoonekana katika (6) na (7):


6. $[\alpha, \ldots\ldots \alpha]$
   $[\beta]$
   ambapo $\beta$ ni {na , au , lakini ...} na $\alpha$ ni kategoria yoyote ya kimiundo

7. $[\alpha\ \beta\ \alpha]$
   $[\beta]$
   ambapo $\beta$ ni {na, au ...} na $\alpha$ ni kategoria ya kimiundo

Hapa, kanuni katika (6) hupachika kiunganishi kama sifa $[\beta]$ kwenye kipashio cha kimiundo kinachokifuata, na kisha kwa kutumia kanuni katika (7), kipashio hicho cha kimiundo hupanuliwa kama inavyoonyeshwa katika (8) kuhusiana na muundo wa KN katika (4):

8. (a) Baba na mama

   (b)





Kwa mujibu wa Gazdar (1981:157), kanuni katika (6) na (7) zilizingatia mapendekezo mengi ya awali lakini ambayo hayakujitosheleza kinadharia kukabili miundo inayojadiliwa hapa, yaani ile yenye viunganishi. Hivyo, pendekezo hili limekitwa katika misingi ambayo

kwa kiasi kikubwa imezoeleka na kukubalika miongoni mwa wanaisimu. Kitu muhimu hapa ni kuwa [β] kama sifa haipaswi kutafsiriwa kama neno kuu (linalomiliki nomino "mama") katika muktadha wa uchanganuzi huu. Yaani, uchanganuzi huu ni tofauti na ule wa Kirai kiunganishi (KU) katika (9) hapa chini ambako kipashio **na** ni neno kuu linalomiliki kijalizo "mama":

9. (a) Ameondoka na mama: Kirai kitenzi (KT) → Kitenzi (T) KU

(b)




Katika (9), kipashio "na mama" ni Kirai kiunganishi (KU) ambacho kipashio "na" mwake ni neno kuu tofauti na "na" katika (8) hapo juu.

Jambo jingine muhimu sasa ni kuona sifa mbalimbali za miundo yenye viunganishi ambazo zitatudhihirishia kuwa, kwa kiasi kikubwa, miundo yote ya aina hii inaweza kuchanganuliwa kwa kanuni katika (6) na (7).

### 3.0 Sifa za miundo yenye viunganishi

Katika sehemu ya Utangulizi, kumeonyeshwa baadhi ya miundo (mifano (2) – (5)) yenye viunganishi. Miongoni mwa miundo hiyo, ile ya Kiingereza katika (2) na (3) ni miundo yenye mapengo yenye viunganishi. Mifano ya miundo kama hii katika Kiswahili tutaionyesha hapa chini. Aidha, ilionyeshwa pia mfano wa muundo wa msingi kabisa wa Kirai Nomino (KN) (katika (4)) ambao nao una kipashio kiunganishi. Vilevile ilionyeshwa muundo (katika (5)) wa sentensi iliyounganishwa lakini isiyokuwa na mapengo.

Baadhi nyingine ya miundo yenye viunganishi iliyowahi kujadiliwa (taz. k.m. Mkude 1982:40-52; Kapinga 1983:187; Ashton 1944:295) ni hii ifuatayo katika (10)-(12):

10. (a) **Juma *na* Musa** wameondoka.
    (b) Binadamu huburudika kwa **kula *na* kunywa**.

11. (a) **Mtoto yule mrefu *na* mjomba wake** wanamtafuta ng'ombe aliyepotea.

(b) Bila shaka **mmenielewa vizuri *na* hamtanisumbua tena**.

12. (a) **Wazazi wanapumzika ndani *na* watoto wanacheza nje**

(b) **Nyie muimbieni *na* wenzenu wampigie makofi** .

Katika mifano hii, sentensi ya (10) huonyesha matumizi ya **na** kuunganisha maneno, yanayounda kirai nomino (kama ule tuliouona katika (4)) wakati katika (11) kiunganishi hicho hutumika kuunganisha virai, na katika (12) huunganisha vishazi . Katika 10(a) kiunganishi hicho kinaunganisha nomino "Juma" na "Musa", hali katika 10(b) kinaunganisha vitenzi "kula" na "kunywa". Katika (11), kwa upande mwingine, **na** huunganisha virai nomino viwili katika (10a) na virai vitenzi viwili katika (11b). Na katika (12) **na** huunganisha vishazi viwili katika (12a) na vingine viwili katika (12b). Ni katika nafasi kama hizo iliko **na** kwenye mifano (10) – (12) ambako kipashio hicho huchukuliwa kuwa na dhima ya kiunganishi kama ilivyodokezwa juu.

Katika nafasi nyingine kama kwenye mifano hii ifuatayo, vipashio **na** na **lakini** huchukuliwa kuwa na dhima tofauti:

13. (a) **Na** iwe hivyo.

(b) **Na** alie tu.

(c) Niletee **na** mimi.

(d) Ameondoka **na** mama.

(e) Amekaa karibu **na** meza.

14. (a) **Lakini** mawazo ya kijana huyo yalikuwa mbali sana.

(b) **Lakini** kwa kiasi fulani fikira haina kipimo.

Mifano hii huonyesha nafasi nyingine katika sentensi vinakoweza kutokea vipashio **na** na **lakini**. Nafasi hizi zi mwanzoni mwa sentensi katika (13a na b) na katika (14a na b) kwa vipashio vyote viwili. Katika (13c–e), kwa upande mwingine, kipashio **na** hutokea kati ya vipashio tofauti tofauti kama vile, kati ya umbo tenzi *niletee* na kiwakilishi *mimi* katika (13c); kati ya umbo tenzi *ameondoka* na nomino *mama* katika (13) na kati ya kielezi *karibu* na nomino *meza* katika (13e).

Mkude (1983:41-52) anachukulia kipashio **na** kuwa na dhima ya "kubainisha hali" katika (13a na b), dhima ya "kihusishi" katika (13d na e) na kama "kiungishi" katika (13c). Anafafanua "kiungishi" kama kipashio "kinacholeta umoja baina ya vipashio ambavyo si lazima viwe na hadhi sawa" (uk. 51). Dhima zote hizi zimefafanuliwa kwa misingi ya kimaana, lakini kimsingi zote zinahusu uunganishaji wa vipashio vya sentensi japo vile visivyo na hadhi sawa kimiundo au vile vilivyo dhahiri na visivyokuwa dhahiri kimiundo. Aidha katika kazi nyingi za awali (taz. k.m. Jacobs na Rosenbaum 1970:253; Longacre 1985:241-246) vipashio ambavyo tumeviainisha kama viunganishi vimeitwa pia kwa majina tofauti kwa misingi ya kimaana. Kwa mfano, kipashio **na**, kimekuwa

kikiitwa "kiunganishi" wakati kipashio au kimekuwa kikiitwa "kitenganishi" kwa misingi hiyo. Hata hivyo, kimiundo, maneno yote katika kundi hili huunganisha vipashio vya sentensi kwa maana ya kuviweka katika muundo mmoja.

Zaidi ya kuunganishwa kwa viunganishi kama hivyo, miundo hii inayohusika pia ina sifa nyingine mbalimbali. Muundo kama ule katika (10) na huwa una sifa ya kuwa muundo wa msingi (kwa maana ya kuwa kiini katika muundo wa sentensi) tofauti na mingine ambayo si kiini na hivyo kutokuwa ya msingi. Kwa mfano, tunachukulia muundo wa Kirai Nomino katika (10a) (yaani fungu "Juma na Musa") kuwa wa msingi[1] tofauti na muundo kama ule uliotanguliwa na "kwa" katika (10b) (yaani fungu "kula na kunywa") ambao umo katika kipashio kisichokuwa cha msingi ndani ya sentensi hiyo (kwa maana ya kuwa maelezo ya ziada yanayoweza kutumiwa au kuachwa). Aidha mifano katika (13) na (14) ni ya miundo ambayo si ya msingi, kwani vinaelekea zaidi kujaliza miundo iliyotangulia ambayo si dhahiri. Hapa pia tunachukulia vipashio kama vile *na mama*, *na mimi*, *na meza*, n.k. kuwa virai viunganishi (taz. k.m. Massamba na Wenzie (1999:112 - 113). Hivi vimekuwa vikijulikana katika sarufi ya Kiswahili kama Virai Viunganishi au Vikundi Vihusishi; na hivyo si vipashio vya msingi.

Aidha katika Kiswahili kuna miundo mingine yenye viunganishi ambayo ni ya aina zifuatazo:

15. (a) Wataondoka *na* wenzao watafuata.
    (b) Najua unanipenda *na* kuniheshimu.
    (c) Mimi *na* yule hatuli meza moja.
    (d) Sijui anavyokula *na* kulala.
    (e) Tembo mwenyekiti *na* sungura katibu.

16. (a) Nilimtafuta *lakini* sikumwona
    (b) Nilifikiri nimpe fedha *lakini* roho haikukubali
    (c) Simpendi *lakini* sina la kufanya
    (d) Si unamwelewa vizuri *lakini*?

17. (a) Atakula *au* ataacha
    (b) Hana hili *au* lile
    (c) Yule jamaa ni mjuzi wa mambo jamani, *au* sio?
    (d) Rudisha fedha zangu *au* utanikoma.

---

[1] Hapa yafaa tutaje kwamba tuna habari na mtazamo unaodai kuwa muundo "Baba na mama wame..." ni muunganiko wa miundo miwili "Baba ame..." na "mama ame...". Lakini nia yetu hapa ni kubainisha tu vipashio vya msingi katika muundo wa sentensi kama vile Kirai Nomino (KN) au Kirai Kitenzi (KT) ambavyo, kwa kawaida, ni lazima vijitokeze katika muundo na vipashio vingine visivyokuwa vya msingi, (yaani vile ambavyo si lazima vijitokeze kila wakati katika muundo) kama vile Kirai Kielezi, n.k.

18. (a) Ana kazi ngumu *tena* ya kuchosha
(b) Kazi anayo *tena* ya heshima
(c) Anaruka kwa nguvu *tena* kwa kasi
(d) Yule kijana ni mwongo *tena* mwizi

19. (a) Sinywi *wala* silewi
(b) Hatumwezi kwa maringo *wala* kwa mbwembwe
(c) Si wewe *wala* mimi mwenye uwezo wa kufanya kazi hii peke yake

Katika mifano (15) hadi (19), viunganishi vyote vimeandikwa kwa hati ya mlazo. Kwa miundo yote iliyoonyeshwa, tofauti ni baina ya ile yenye mapengo na ile isiyokuwa na mapengo. Kama tulivyodokeza awali, miundo yenye mapengo ni ile ambamo kipashio kilichostahili kurudiwa hasa baada ya kiunganishi, kinadondoshwa. Mifano ya miundo yenye mapengo ni (17 b na c), (18 a–d) na (19 b na c). Ndani ya miundo hii tunaweza kujumuisha ile katika (15 b na d) ambamo maumbo tenzi yanayofuata viunganishi yana kiambishi **ku**. Katika miundo hii napo, vishazi vinavyoundwa na maumbo tenzi yenye kiambishi **ku** haviwezi kujitegemea. Miundo yenye mapengo katika Kiswahili haijawahi kuchunguzwa sana[2], na hadi hivi sasa tunaweza kuhusisha mapengo na aina moja tu ya miundo katika Kiswahili. Na hata hapa tunachoweza kusema tu ni kwamba yanafungamana zaidi na miundo yenye viunganishi *au*, *wala* na *tena*. Katika lugha kama Kiingereza, miundo hii hufungamana zaidi na kiunganishi *na*. Lakini cha muhimu zaidi kuhusiana na miundo hii ni kwamba uchanganuzi wake unahitaji mbinu changamani zaidi, kwani, kwa hakika, hii ni jamii ya miundo changamani katika lugha . Zaidi ya hayo, katika muundo kama (16d) kipashio *lakini* ambacho tumekiainisha kama kiunganishi, kinaweza pia kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Kikiwa mwanzoni mwa sentensi, kinafanya muundo ufanane kwa kila hali na ile katika (14 a na b) juu. Miundo mingine yote inayobaki katika mifano hii ni ile isiyokuwa na mapengo. Katika miundo hii kila kishazi kilichounganishwa ki huru kwa maana kwamba kikiondolewa katika muktadha wa sentensi kubwa kinaweza kujitegemea.

Kwa hiyo, kulingana na data tuliyo nayo, na tukiacha kando suala la baadhi ya vipashio katika sentensi husika kuwa vya msingi au visivyo vya msingi, sifa nyingine muhimu ya miundo yenye viunganishi ni ile ya kuwa au kutokuwa na mapengo. Tumeona vilevile kwamba kiunganishi kinaweza kuwa tu kinahusisha muundo usiokuwa wa msingi na mwingine usiokuwa dhahiri. Lakini pamoja na sifa hizi, tumeamua kuzingatia mtazamo unaochukulia kiunganishi kuwa sehemu ya kifundo kinachokifuata katika muundo hasa ile isiyokuwa na mapengo.

---


[1] Uchunguzi tu uliopo ni ule wa Khamisi (1988:120-133) unaohusu zaidi virai nomino visivyojitokeza dhahiri lakini ambavyo vinawakilishwa na viambishi katika maumbo tenzi.

Hata hivyo, kiunzi cha Miundo Virai Changamani kilichotajwa hapo katika sehemu ya (2) juu kinagawanya miundo yote yenye viunganishi katika makundi mawili makuu. Haya ni ya "Miundo Iliyounganishwa" [*Coordinate Structure*] na "Miundo Isiyounganishwa" [*Unbounded Dependencies Constructions*]. Kundi la kwanza ndilo la miundo ambayo, kwa kawaida, inajulikana kama "Sentensi Ambatani" (k.m. miundo katika (5), (12), (15a), (16a), (17a) na (19a)) ambazo ndani mwake mmeunganishwa vishazi huru. Vishazi huru ni vile ambavyo vikiondolewa kwenye muktadha wa sentensi kubwa, huweza kujitegemea kama sentensi huru. Kundi la pili, kwa upande mwingine, ni la aina mbalimbali za miundo inayojulikana kwa jumla kama "Sentensi Changamani"; ila katika muktadha wa miundo inayojadiliwa hapa, aina inayohusika hasa ni ile ya miundo yenye viunganishi na mapengo ndani mwake kama ilivyodokezwa hapo juu. Kwa kawaida, kishazi chenye pengo katika miundo kama hii huwa hakiwezi kujitegemea; lakini hutegemeana na chenzake. Hii ndiyo sababu miundo hii huitwa miundo isiyounganishwa. Kiunzi cha Sarufi Miundo Virai Changamani hutambua pia uunganishaji katika kiwango cha virai tofauti na kiunzi cha Sarufi Geuza-maumbo Zalishi ambacho katika kanuni yake katika (1) juu hakitambui uunganishi katika kiwango hicho.

Kwa minajili ya maelezo haya, tunafikiri miundo mbalimbali iliyounganishwa inaweza kuchanganuliwa kwa kufunganisha kipashio kiunganishi na kipashio kinachofuata. Hii ina maana kwamba muundo wa Sentensi ambatani katika (6) na (7):

20. (a) Mama anafagia na watoto wake wanacheza nje

(b)




## 4.0 Hitimisho

Kama tulivyoona katika sehemu ya **2** hapo juu, kanuni katika (6) na ile katika (7) zinaweza kutumiwa kuchanganua miundo yote yenye viunganishi. Hii inaweza kuwa ni pamoja na miundo yenye viunganishi yenye mapengo. Ila katika miundo hii yenye mapengo huhitajika kanuni nyingine ya kubainisha pale lilipo pengo. Si nia yetu sasa kuingia mawanda ya mapengo katika miundo, kwani hiyo inaweza kutuingiza pia katika

uchanganuzi wa miundo yote yenye mapengo iliyounganishwa na isiyounganishwa. Kazi kama hiyo tunafikiri inaweza ikafanyika katika makala mengine yatakayofuata. Katika makala hii, tumejaribu kuonyesha kuwa kuna mapendekezo mengine ya kuchanganua miundo yenye viunganishi ambayo ni kanuni katika (6) na (7). Kanuni hizi kama tulivyoona katika sehemu ya 2 hapo juu yanakifunganisha kipashio kiunganishi na kipashio cha kimiundo kinachokifuata katika mpangilio kwenye muundo. Hii, kimsingi, inatuondoa katika matatizo ya kinadharia yaliyoibuka kutokana na matumizi ya kanuni katika (1) iliyopendekezwa na kiunzi cha nadharia ya Sarufi Geuza-maumbo Zalishi.

## MAREJEO


Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar and Intonation* Longman, uk. 398.

Gazdar, G. (1980). "A Cross-categorial Semantics for Coordination", *Linguistics andPhilosophy* 3, kur. 407-409.

(1981). "Unbounded Dependencies and Coordinate Structure". Katika *Linguistic Inquiry* Juz. 12 Na. 2 kur. 155-184.

Gazdar, G. na wenziwe (1982). "Coordination and Transformational Grammar". Katika *LinguisticInquiry* Juz.. 13 Na. 4 kur. 663–677.

Kapinga, M. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI.

Keenan, E. L. na L. Faltz (1978). "Logical Types for Natural Language". Katika *UCLA Occasional Papers in Linguistics* 3.

Khamisi, A. M. (1988). "A Typology of Gaps in Kiswahili Sentences". Katika *Kiswahili* Juz. 55/1&2 kur. 120–133.

Longacre, R.E. (1985). "Sentences as combinations of clauses". Katika T. Shopen (Mh.) *Language Typology and Syntactic Description* (LTSD), CUP Juz. Na. 3 kur. 235 –285.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. London: CUP.

Massamba, D. P. B. na wenzie (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA)Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mkude, D. (1983). "Matumizi ya 'Na' katika Kiswahili". Katika *Mulika* Na. 15 kur. 40–52.

Ross, J. (1967). "Constraints on Variables in Syntax". Doctoral Dissertation, MIT.

Sag, I.A. (1982). "Coordination, Extraction and Generalized Phrase Structure Grammar". Katika *Linguistic Inquiry*, Juz. 13 Na.2 kur. 329–336.

Schachter, P. (1976). "A Nontransformational Account of Gerundive Nominals in English". Katika *Linguistic Inquiry* 7, kur 205-241.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Van Oirsouw, R.R. (1982). "Gazdar on Coordination and Constituents". Katika *Linguistic Inquiry* Juz. 13 na. 3, kur. 553–557.